INS-P006- KUCHUNGUZA RIPOTI YA UONEVU KWA MWANAFUNZI, UNYANYASAJI, VITISHO, UONEVU, UNYANYASAJI WA MTANDAONI NA VURUGU KWENYE URAFIKI WA MAPENZI KWA VIJANA

UTARATIBU

MAELEKEZO

MUHTASARI

Utaratibu huu unaelezea mchakato wa kuripoti na kuchunguza ripoti ya uonevu, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandaoni na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana na vitisho vinavyohusisha wanafunzi. Utaratibu wa kutoa ripoti na uchunguzu unyanyasaji wa kijinsia unaohusisha wanafunzi umeainishwa katikaINS-P032. Utaratibu wa kuripoti na kuchunga matukio ya upendeleo na alama za chuki umeainishwa katka ADM-P012

MAANA

STAT

Timu ya Kutathmini Vitisho kwa Mwanafunzi

SIRC

Kamati ya Kujibu Matukio ya Ngono

SPP

Itifaki ya Kuzuia Kujiua

MAELEKEZO

1. . Mkuu wa shule hupokea riporti zote za uonevu, unyanyasaji, vitisho, uonevu, unyanyasaji wa mtandao na/au vitisho
    a. Wafanyakazi wote wa wilaya ya shule watoe ripoti kuhusiana na uonevu, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandao na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana moja kwa moja kwa mkuu wa shule kwa maneno au kwa maandashi.
        i. . Ripoti zinaweza kutokana na uchunguzi wa moja kwa moja kutoka kwa mfanyakazi kwa kuangalia, taarifa kutoka kwa wanafunzi au wazazi au kutoka sehemu nyingine.
    b. Wanafunzi wanahimizwa kutoa taarifa ya wasiwasi wowote kuhusiana na uonevu, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandao, vurugu kwenye urafiki wa mapenzi na vijana, na/au vitisho kwa kufanya moja ya yafuatayo:
        i. Kukamilisha Ripoti ya Siri ya Mwanafunzi iliyoko ofisini au kituo cha ushauri; au
        ii. Muone Mwalimu mkuu, msaidizi wa Mwalimu mkuu, mshauri wa wanafuzi, mtu wa tabia au mtu unayemwamini shuleni au kwenye Idara; au
        iii. Toa ripoti kwa SafeOregon Kuwapatia taarifa; Piga au ujumbe kwa maneno 844-472-3367, email tip@safeoregon.com au tembelea www.safeoregon.com. Taarifa inaweza kutolewa bila kujitambulisha.
    c. Walezi na wanajamii wanahimizwa kuwasilisha malalamiko kwa kukutana na msimamizi wa shule. Watu binafsi wanaweza pia kuwasilisha malalamiko rasmi kama ilivyoainishwa katika ADM-P008.
2. Mkuu wa shule ana jukumu kuu la kuchukunguza kila ripoti : ya uonevu, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandao na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana na vitisho vinavyohusisha wanafunzi lakini anaweza kuteua mteule au kuhusisha wafanyakazi wengine wa wilaya kama inavyofaa ili kuhakikisha hatua zifuatazo zinakamilika ikiwa inatumika.
    a. Wataarifu wakala wa kutekeleza sheria juu ya shughuli zinazowezekana za uhalifu, pamoja na lakini sio tu unyanyasaji wa watoto, unyanyasaji wa kimwili, au uharibifu wa mali.
    b. Tekeleza hatua za muda ili kusaidia kuhakikisha usalama wa wanafunzi wakati wa uchunguzi.

c. Anzisha itifaki ya tathmini kwa tishio la wanafunzi (STAT) itifaki ya kukubaliana na matukio ya ngono. (SIRC) au itifaki ya kuzuia kujiua(SPP)
d. Mjulishe mratibu wa Title IX kama mwenendo ulioripotiwa unaweza kukiuka Title IX.
e. Mjulishe mratibu wa usafiri au meneja wa wilaya ya shule kwenye idara ya usafiri kama tukio lilitokea kwenye usafiri ulioruhusiwa na wilaya au kwenye kituo husika cha basi.
f. Hifadhi rekodi juu ya malalamiko yote pamoja na nyaraka zilizoandikwa za uchunguzi.

3. Uchunguzi lazima Ujumuishe:
    a. Mahojiano yanamuhusisha wanafunzi, watu wazima wenye taarifa, mashahidi na wengine wanaochukuliwa kuwa wanafaa na mkuu wa shule au mtu aliyetuliwa.
        i. Mahojiano na watu waliohusika na shahidi watafanyika tofauti (mfano; shahidi atahojiwa pekee badala ya kuhojiwa pamoja na kundi).
        ii. Wilaya ya shule itajitahidi kutunza utambulisho wa mtu kuwa ni siri, lakini mtu anayefanya uchunguzi hatakiwi kuahidi kuwa itakuwa ni siri. Utambulisho wa mtu wakati mwingine unaweza kuhitajika kisheria au kwenye mkataba wa kikazi na mwajiri.
    b. Pitia Ushahidi wote uliopo.
4. Mkuu wa shule atahakikisha taarifa imewafikia wazazi/wanalezi wa mwanafunzi ambaye alifanyiwa kitendo cha ya uonevu, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandao na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana na vitisho vinavyohusisha wanafunzi.
    a. Taarifa lazima itolewe kwa kuhusisha na kuzingatia mahitaji na wasiwasi wa mwanafunzi ambaye alifanyiwa ya uonevu, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandao na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana na vitisho vinavyohusisha wanafunzi au kitendo cha unyanyasaji wa mtandao.
    b. Taarifa haitakiwi kama mkuu wa shule anaamini kwamba kwa kutoa taarifa kunaweza kuhatarisha maisha ya mwanafunzi ambaye alifanyiwa vitendo vya ya uonevu, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandao na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana na vitisho vinavyohusisha wanafunzi au kitendo cha unyanyasaji wa mtandao.
        i. Mwanafunzi ambaye alifanyiwa kitendo hicho anaomba kwamba taarifa isitolewe kwa wazazi/walezi wa mwanafunzi;
        ii. Mkuu wa shule anaamua kuwa taarifa sio kwa maslahi ya mwanafunzi ambaye alifanyiwa kitendo hicho; na
        iii. Mkuu wa shule anamjulisha mwanafunzi kwamba sheria ya shirikizo inaweza kuhitaji wazazi au walezi wa mwanafunzi kupata rekodi ya elimu ya mwanafunzi ikiwa ni pamoja na maombi yoyote yaliyotelewa kama ilivyotolewa katika sehemu hii.
    c. Ikiwa mkuu wa shule hatafanya uamuzi ulioanishwa katika 4. b... mkuu wa shule lazima kutoa taarifa kwa mwanafunzi kabla ya kuwajulisha wazazi/walezi wake.
    d. Wakati taarifa inatolewa chini ya kipengele hiki, taarifa lazima itolewe:
        i. Ndani ya muda unaofaa au
        ii. Ambapo pale vitendo ambavyo vilisababisha madhara ya mwili wa mwanafunzi
5. Mwisho mwa uchunguzi, mkuu au aliyechaguliwa atafanya:
    a. Mjulishe mwanafunzi na ikiwa inakubalika wazazi/walezi wa mwanafunzi kuhusu matokeo ya uchunguzi.
    b. Anzisha mazoea ya kurejesha na/au nidhamu kama ilivyoanishwa katika sera na taratibu za Wilaya ya shule kwenye ya uonevu, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandao na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana na vitisho vinavyohusisha wanafunzi kama ilivyoonyesha kwenye INS-A003.

MATUMIZI

- Wanafanyakazi na wanafunzi wote wa SKPS

NYARAKA ZINAZOHUSIANA

- INS-A003- Uonevu wa mwanafunzi, unyanyasaji, vitisho, unyanyasaji wa mtandao na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana na vitisho vinavyohusisha wanafunzi.
- PAP-A001- Unyanyasaji wa Watoto na Mwenendo wa Kijinsia
- ADM-P008- Malalamiko, Umma: Mchakato wa Kutatua
- INS-F030- Ripoti ya Mwanafunzi na Unyanyasaji na Uonevu
- ADM-P010- Kuchunguza Ripoti za Matukio ya Upendeleo na Alama za Chuki
- INS-P032- Kuchunguza Ripoti za Unyanyasaji wa Kinjisia: Wanafunzi

MAMLAKA YA INDHINI

- Naibu Msimamizi wa Mashule

HISTORIA YA MAREKEBISHO

- 09/04/2013 Imeongeza neno aliyeteuliwa kwenye kipengele cha 2.3 na mabadiliko mengine madogo ya lugha.
- 10/10/2014 - Ongeza Kipengele 4.4 kuonyesha Ripoti ya Siri ya Mwanafunzi
- 06/03/2019 - Sehemu za 2.1 na 2.2 zilizosasishwa ili kuendana na kanuni mpya na vidokezo vya kuripoti
- 12/08/2020 - Taarifa zilizojumuisha kuhusu ADM-P010; sasisho kwa 2.1.1, 2.3.1.1, 2.3.1.2 na 2.4.2
- 07/26/2021 – Imeongeza kipengele kipya (2.4) inayoelezea hatua za kutoa taarifa kwa wazazi/walezi.
- 09/20/2021 - Rejea sasisho ya itifaki ya kuzuia kujiua katika kipengele cha 2.2.3.
- 03/26/2026 - Imeongeza Vurugu za Urafiki wa mapenzi kwa Vijana wote, kuongeza taarifa kwa Mratibu wa Title IX iliyohamishiwa kwenye templeti inayoweza kufikiwa.